

SHERIA NA HAKI

Kwa kila mwananchi



ISSN 0000 - 0000

Toleo Na.003

Jarida la kila miezi mitatu

Julai - Septemba 2010

ZLSC kuangalia Uchaguzi

TUME ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC) imekiruhusu Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC) kufuatilia na kutazama zoezi la Uchaguzi Mkuu wa Zanzibar.

Afisa wa Mipango wa ZLSC, Bi Harusi Miraji Mpatani, amesema ZEC imetoa kibali cha kuangalia uchaguzi tokea zoezi la uandikishaji, kampeni, upigaji kura na uhesabuji wa kura katika majimbo yote ya uchaguzi. ZEC imapanga Oktoba 31, 2010, kuwa siku ya kupiga kura.

Alisema ZLSC itawatumia wasaidizi wake wa sheria (paralegals) waliopo katika majimbo 50 ya uchaguzi, majimbo 32 yapo Unguja na 18 yapo Pemba, kufuatilia harakati zote za uchaguzi na kila mmoja kutoa ripoti yake.

Hii ni mara ya nne kwa ZLSC kusimamia zoezi la Uchaguzi Mkuu wa Zanzibar wa vyama vingi. Mara ya kwanza ZLSC chini ya Kikundi cha Kufuatilia na Kutazama Uchaguzi wa Zanzibar (ZEMOG) ilisimamia zoezi la Uchaguzi Mkuu wa Zanzibar

Inaendelea Uk.15



Baadhi ya waangalizi wa ndani na wa nje wa uchaguzi wa Zanzibar wakijadili jambo.

Adhabu ya kifo katika uislamu

KITABU kinachozungumza kuhusu Adhabu ya Kifo kwa mujibu wa sheria ya Dini ya Kiislamu kinatarajiwa kuzinduliwa

Oktoba 10 ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya siku ya Adhabu ya Kifo Duniani.

Taarifa iliyotolewa na Kituo cha

Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC) imesema

kwamba kitabu hicho kimeandikwa na mwanachuoni maarufu Zanzibar, Sheikh Muhidd Ahmad Khamis.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, kitabu hicho kimeandikwa kwa lugha ya Kiswahili na kimetafsiriwa kwa lugha ya Kiingereza. Uzinduzi wa Kitabu hicho utakwenda sambamba na semina ya siku moja zitakazotayarishwa na ZLSC kujadili adhabu ya kifo

Wanaharakati wa haki ya binadamu wanaendeleza kampeni dhidi ya adhabu ya kifo kwasababu niikatili na kinyume na haki za



Sheikh Dkt. Muhidin Ahmed Khamis akizungumzia adhabu ya kifo katika uislamu.

Inaendelea Uk.15